

MAKAO MAKUU

**Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania**

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa
Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya kusambaza umeme kutoka kwa Kampuni iliyotajwa hapo chini. EWURA inakaribisha maoni na/au pingamizi kuhusiana na maombi haya. Taarifa za muombaji pamoja na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:

Na.	MAELEZO
Jina na anuani ya Mwombaji	Mwenga Power Services Limited. Kiwanja Na. 18, Eneo la Vingunguti, Barabara ya Nyerere , Dar es Salaam. S. L. P 70192, Dar es Salaam.
Eneo	Kata za Luponde na Iwungilo, Wilaya ya Njombe Mjini, Mkoa wa Njombe; na Kata ya Suma, Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya.
Taarifa za Wanahisa	1) Rift Valley Energy Tanzania Ltd, Kiwanja Na.18, Eneo la Vingunguti, S. L. P 70192, Dar es Salaam, 99% ; na 2) Highland Tea Company Ltd, Ghorofa ya 1, Jengo la Hidary Plaza S. L. P 70192, Dar es Salaam, 1%
Maelezo ya Mtambo na	1) Miundombinu ya usambazaji umeme, kwa ajili ya kusambaza umeme kwenye vijiji saba (7), ambavyo ni Lusitu, Miva, Igola,

Matumizi	<p>Iduchu, Luhololo, Uliwa na Luponde, vilivyopo kwenye kata za Luponde na Iwungilo. Umeme utakao sambazwa utazalishwa na Mtambo wa kufua umeme kwa kutumia maji wa Luponde utakaokuwa na uwezo wa Megawati 2.9.</p> <p>2) Miundombinu ya usambazaji umeme, kwa ajili ya kusambaza umeme kwenye vijiji vinne (4), ambavyo ni Malamba, Suma, Busona na Bunyakikosi vilivyopo kwenye kata ya Suma. Umeme utakaosambazwa utazalishwa na Mtambo wa kufua umeme kwa kutumia maji wa Suma utakaokuwa na uwezo wa Megawati 1.5.</p>
Aina na Muda wa Leseni	Leseni ya Muda Mfupi ya Kusambaza Umeme ya Miaka mitatu

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi haya awasilishe kwa maandishi kabla ya saa 10 jioni, siku ya tarehe 27 mwezi Aprili, 2018. Maombi ya leseni yanaweza kuonyeshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu